



JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb Na: HWP/A.10/5/19

10/03/2022

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI YA MAKAZI NA POSTIKODI HALMASHAURI YA PANGANI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika Mitaa na Vitongoji vyote vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Pangani.

A) SIFA ZA WAOMBAJI.

- i) Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35.
- ii) Awe Mkazi wa Halamshauri ya Wilaya ya Pangani.
- iii) Awe na Elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- iv) Awe anamiliki Simu janja (Smartphone) inayotumia mfumo wa uendeshaji wa android (Android OS) yenye uwezo wa kukaa na chaji siku nzima (masaa ishirini na nne).
- v) Awe na uwezo wa kusoma/kutafsiri ramani za mitaa/Kitongoji.
- vi) Awe ni mkazi wa Kata/Kijiji/Kitongoji husika.
- vii) Awe tayari kufanya kazi katika kata yeyote ndani ya Halmashauri ya Pangani.

S.L.P 89 Pangani, Simu 027 2977485, Barua Pepe ded@panganidc.go.tz, Tovuti
www.panganidc.go.tz

B) KAZI NA MAJUKUMU.

1. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja, na maeneo ya huduma.
2. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja, na maeneo ya huduma kwa kutumia programu tumizi ya mfumo wa anwani za makazi.
3. Kutuma data kwenye mfumo wa anwani za makazi.
4. Muda wa kazi Utazingatia Mkataba wa kazi.

C) MAOMBI YAAMBATANISHWE NA;

- i) Nakala ya cheti cha Kidato cha nne na kuendelea.
- ii) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- iii) Picha mbili za Passport size.
- iv) Barua ya maombi ipitie kwa Mtendaji wa kijiji na kata anapoishi.

D) JINSI YA KUTUMA MAOMBI.

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu inayopatikana muda wote, pamoja na barua pepe (Email) inayofanya kazi na kuwasilishwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Pangani kwa anwani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA PANGANI,
S.L.P 89.


PANGANI.

S.L.P 89 Pangani, Simu 027 2977485, Barua Pepe ded@panganidc.go.tz, Tovuti
www.panganidc.go.tz

Aidha chini ya Bahasha upande wa kulia iandikwe OAZM/PDC/2022/001.

E) TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20/03/2022 saa 9.30 Alasiri.



JORAM .A. NOA

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA

PANGANI.

**KAIMU MKURUGENZI
MTENDAJI (W) PANGANI**

S.L.P 89 Pangani, Simu 027 2977485, Barua Pepe ded@panganidc.go.tz, Tovuti
www.panganidc.go.tz